



Parna alikuwa  
mvulana mwembamba  
mrefu.

Alikuwa katika darasa  
la tatu.

Alipenda kuvalaa koti  
refu la rangi nyeusi.  
Alipewa koti hilo na  
Mjombake, Teteyo.



Wakati wa likizo, Parna  
aliwachunga ng'ombe  
wa wazazi wake.



Siku moja, Parna  
alikuwa akiwachunga  
ng'ombe. Ghafla,  
mvua ilianza  
kunyesha.



Wakati huo huo,  
Cheusi, ng'ombe  
aliyekuwa kipenzi cha  
babake, alizaa.

Ndama aliyezaliwa  
alipendeza. Alikuwa  
mzuri kuliko ndama  
wote ambao Parna  
aliwahi kuwaona.



Parna alifurahi  
kuwahudumia Cheusi  
na ndama wake.  
Aliwasahau ng'ombe  
wale wengine.



Aliwaza, "Babangu  
aliahidi kunipa ndama  
ikiwa atakuwa wa  
kike."



Alipokuwa akiwaza hivyo, alisikia mkono ukimvuta juu kwa nguvu.

Parna alimwona Mjomba Teteyo.  
Alikumbuka na kuuliza,  
"Mjomba, ng'ombe wako wapi?"




Mjomba Teteyo  
alimjibu, "Mamako  
aliwapata ng'ombe  
wote zizini ila wewe na  
Cheusi. Aliingiwa na  
wasiwasi akanitura  
nije nikuchukue."




Mjomba Teteyo  
akasema, "Nitambeba  
ndama huyu. Kisha  
wewe na Cheusi  
mnifuate nyuma."


Parna alielezea kwa  
msisimko jinsi Cheusi  
alivyozaa ndama aliye  
mzuri zaidi ya wote.



Watu wote walifurahi  
walipoona kwamba  
Parna, Cheusi na  
ndama walikuwa  
salama.



Parna akamwuliza  
babake, "Je, utanipa  
ndama huyu kama  
ulivyoahidi?"



"Ndiyo, mwanangu,  
ndama huyu ni wako.  
Ahadi ni deni."